

SIKU YA FIGO DUNIANI, WATU KIBAO WAJITOKESA KUPATA HEDUMA HOSPITALI YA RUFAA MBEYA LEO



Kaimu kurugenzi wa Hospitali ya Rufaa Mbeya Daktari Omari Salehe akiongozana na mgeni rasmi Meya wa jiji la Mbeya Athanas Kapunga kwenda kuangalia vifaa mbalimbali vya kupimia figo



Dkt Octabenny Kassanga akitoa maelezo kwa meya wa jiji la Mbeya
jinsi vifaa hivyo vinavyofanya kazi



Daktari Onesmo Kisanga kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.
katikati akimfafanulia jambo meya wa jiji Athanas Kapunga







Wananchi mbali mbali wa Mbeya wakiwa wamejitokeza kwa wingi katika upimaji figo bure





Meya wa Jiji la Mbeya Athanas Kapunga ameishukuru Serikali kwa kuiwezesha Hospitali ya Rufaa Mbeya kupata vifaa vya kupimia magonjwa ya figo.

Kauli hiyo ameitoa katika Hospitali ya Rufaa Mbeya katika maadhimihiyo ya siku ya figo nchini ambapo wakazi wa Mbeya wamejitokeza kupima ili kujua Afya zao na maadhimihiyo hayo yamehudhuriwa na Daktari Onesmo Kisanga kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

Kisanga ambaye ni Rais wa Madaktari wa figo nchini amesema hivi sasa kumekuwa na ongezeko la wagonjwa wa figo kila siku hiyo inatokana na wananchi wengi kutopima afya zao hali ambayo ingeweza kuzuia matatizo makubwa ambayo hupelekea gharama kubwa za upasuaji.

Aidha Daktari bingwa amesema pia uhaba wa Madktari wa fani hiyo unawafanya waliopo kupata msongamano mkubwa wa wagonjwa kutoka mikoani pia wengi kofahamu kuwa hivi sasa Serikali imesogezza huduma hiyo katika Hospitali za Rufaa ikiwemo Mbeya yenyе madaktari watatu wa figo.

Kati ya Madaktari watatu wawili ni raia wa Cuba na mmoja ni Mzalendo anayefahamika kwa jina la Octabenny Kassanga ambaye amewataka wananchi wa Mbeya kufika Hospitali ili waweze kujua Afya zao na kupatiwa tiba sahihi na ushauri ili kudhibiti ongezeko la

ugonjwa huo ambao ukicheleweshwa gharama zake ni kubwa ambazo na zaidi ya shilingi milioni ishirini.

Kaimu kurugenzi wa Hospitali ya Rufaa Mbeya Daktari Omari Salehe amewataka wananchi kujitokeza kwa wingi katika Hospitali ya Rufaa ili kuokoa gharama kwani wanazo mashine za kisasa pia mdaktari waliobobea katika fani ya magonjwa ya figo ambapo katika siku mbili wagonjwa watapatiwa huduma ya vipimo bure kuanzia Machi 12 hadi Machi 14 mwaka huu.

Na Mbeya yetu

1

Posted by Mbeya Yetu at 1:22 PM No comments: [►](#)

[g+1](#) Recommend this on Google

MRADI MPYA WA KIHUMBE WA KITUO CHA KUKUZA UJUZI KWA VITENDO WAZINDULIWA MBEYA



Mkuu wa Wilaya ya Mbeya Norman Sigala alipokuwa anazindua mpango wa kuwajengea uwezo wanafunzi 60 waliomaliza mafunzo ya ushonaji na ufundi magari baada ya kupata msaada wa vifaa vipyanya kisasa kutoka shirika la IMARISHA la Marekani.